

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S.L.P 1951  
Moshi

**TAARIFA KWA UMMA**

**KILIMANJARO 03/02/2020**

**MWENYEKITI NA MTENDAJI WA KIJJI MBARONI KWA RUSHWA**

Mwenyekiti wa kijiji cha Ruvu Jiungeni Kilaseko Sokoine na mtendaji wa kijiji hicho Mohamed Sanja wamekamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoani Kilimanjaro kwa tuhuma za kuomba rushwa ya shilingi milioni moja(1,000,000/=) na kupokea rushwa ya shilingi laki saba (700,000/=)

Tukio la kukamatwa kwa watumishi hao wa umma lilitokea tarehe Januari 30, 2020 baada ya kuwekewa mtego na maafisa wa TAKUKURU huko Ruvu Jiungeni wilayani Same

Uchunguzi wa TAKUKURU unaonyesha kwamba kabla ya kukamatwa kwao,walituma Kamati ya Uchumi na Mipango ya Kijiji cha Ruvu Jiungeni kwenda kitongoji cha MVUNGWE kupima shamba la ukoo wa Ndorosi lililokuwa likidaiwa kuwa kubwa kuliko walilopewa na Serikali ya kijiji mwaka 2008

Wajumbe wa kamati walirejesha taarifa kwa Kilaseko Sokoine na Mohamed Sanja kuwa kazi ya kupima shamba haikufanyika kwa kuwa walitishiwa kupigwa na wamiliki wa shamba hilo. Sokoine aliwaita ndugu watatu wa ukoo huo na akawapeleka kituo cha Polisi Makanya ambapo aliwafungulia jalada la kutaka kusababisha uvunjiwa wa amani na wakadhaminiwa

Huku wakifahamu kuwa lalamiko hilo wamekwishalifikisha Polisi, Sokoine kwa kushirikiana na Mohamed Sanja waliwaita ndugu hao watatu na kuwataka wadhaminiwe tena ofisi ya kijiji,

kisha wakawataka kutoa fedha shilingi laki tisa (900,000/=) ili wasiwachukulie hatua zaidi za kisheria. Ndugu hao watatu walitoa taarifa TAKUKURU iliyowezesha kukamatwa kwa Mwenyekiti huyo wa kijiji na Katibu wake wakiwa wamepokea fedha hizo,

**Mara uchunguzi utakapokamilika watahumiwa wote wawili watafikishwa mahakamani ili sheria iweze kuchukua mkondo wake na tunatoa rai kwa watanzania waendeleo kutuunga mkono kwa kutoa taarifa za rushwa kila wanapodaiwa**

Imetolewa na

HOLLE J. MAKUNGU  
MKUU WA TAKUKURU (M)  
KILIMANJARO